JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# KANUNI KUHUSU MAADILI YA MADIWANI

***(Mada iliyoandaliwa kwa ajili ya Semina ya Madiwani, Januari 2006)***

**Dodoma**
**Januari, 2006**

# KANUNI KUHUSU MAADILI YA MADIWANI

## Utangulizi

1. Chimbuko la viongozi wa umma kutakiwa kuwa na maadili mema ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

   – Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza kuundwa kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na pia kutungwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma itakayozingatiwa na viongozi wote wa umma.

   – Katiba ya Jamhuri, pia, imeweka misingi ya maadili ya viongozi wa umma ambayo ni pamoja na viongozi wa umma kutakiwa kutoa mara kwa mara tamko la mapato, rasilimali na madeni yao na inawataka viongozi wasiwe na tabia ya udanganyifu, upendeleo, au ukosefu wa uadilifu au tabia inayochochea rushwa wakati wanatekeleza shughuli za umma.

2. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawataka viongozi wa umma wawe na uaminifu, wawe wawazi, wenye kutoa haki bila upendeleo, walinde fedha na mali ya umma na iwapo hawatekelezi jukumu hilo wafukuzwe au kuondolewa madarakani.

3. Bunge kwa kufuatia maelekezo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Na.13/1995) ambayo inawataja Meya, Mwenyekiti, Wajumbe wa Halmashauri ya Wilaya, ilivyorekebishwa na sheria Na. 5 ya mwaka 2001 Mji, Manispaa na Jiji na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwa baadhi ya viongozi wanaotakiwa kutekeleza maagizo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo yamefafanuliwa katika sheria hiyo ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

4. Licha ya maagizo hayo ya Katiba, Sheria za Serikali za Mitaa Na.7/82 na Na.8/82 zimempa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa uwezo wa kutunga Kanuni za Maadili ya Madiwani kwa lengo hilo hilo la kutekeleza maagizo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na uwezo huo uliotolewa kwake, Waziri, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwepo maadili mema katika uendeshaji wa Serikali za Mitaa tayari ameishatunga chini ya Vifungu 170A na 109A vya Sheria Na.7/1982 na Na.8/1982 kwa mfuatano, Kanuni za Maadili ya Madiwani za mwaka 2000 ambazo Mameya, Wenyeviti na wajumbe wote wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji wanapaswa kutekeleza.

5. Maadili mema ya madiwani ni sharti muhimu sana katika kuweka mahusiano mema kati ya Halmashauri, Wananchi na watendaji ili kujenga imani ya Wananchi kwa viongozi wao wa umma na kwa Halmashauri zao. Diwani ni kiongozi wa ngazi ya juu katika ngazi ya wilaya; miji, manispaa na jiji na, kama kiongozi, wananchi wana haki ya kutegemea kuwa atatoa mfano wa kuigwa katika maisha yake ya kila siku na katika utekelezaji wa majukumu aliyokabidhiwa kwa mujibu wa sheria.

6. Kwa upande mwingine ni ukweli usiofichika kuwa wananchi hujali na kuheshimu zaidi uongozi unaothibitishwa na matendo mema pamoja na mwenendo mzuri wa viongozi na watumishi wao na sio tu kwa ufasaha wa kauli au ahadi wanazotoa.

7. Kanuni za Maadili ya Madiwani zinazingatia misingi ifuatayo:

- Kujenga na kudumisha imani ya wananchi kwa viongozi wao;
- Kuweka utaratibu mzuri wa uwazi na uwajibikaji;
- Kujenga mazingira bora ya kuwavutia wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo katika maeneo yao;
- Kupunguza migongano kati ya madiwani, watendaji na wananchi;
- Kuweka bayana maadili yanayotegemewa kwa viongozi katika jamii ya watu; na
- Kuibua na kudumisha demokrasia.

**Misingi, Taswira na Malengo ya Kanuni za Maadili ya Madiwani**

8. Msingi mkuu ulio katika kanuni hizi ni ule unaosisitiza utumishi, uwakilishi na maslahi ya wananchi kwa ujumla badala ya maslahi ya binafsi. Kufuatana na msingi huu Diwani wa Halmashauri anatakiwa kuzingatia kiwango cha juu kabisa cha maadili yanayojumuisha tabia yake binafsi na mwenendo wa utendaji wa majukumu ya kazi yake, yaani:

(a) kuendesha shughuli zake kwa namna itakayojenga imani ya wananchi kwa Halmashauri yao;

(b) kuheshimu na kuzingatia sheria na kuendesha shughuli zake kufuatana na dhamana aliyopewa na wananchi;

(c) kuisaidia Halmashauri yake kwa kadiri iwezekanavyo kuhakikisha kuwa inatekeleza wajibu wake kwa kuzingatia maslahi ya jamii nzima;

(d) kutotumia nafasi yake kama Diwani wa Halmashauri kwa faida yake mwenyewe, ya familia yake, maslahi ya kifedha ya marafiki zake, na kutotoa upendeleo wa aina yoyote wakati wa kutekeleza majukumu yake;

(e) kutojiweka katika hali itakayowafanya wananchi kubishia uadilifu wake;

(f) kuwajibika ipasavyo kwa wananchi walio kwenye eneo la Halmashauri yake kutokana na maamuzi na matendo yake;

(g) kuwa mu-wazi katika matendo yake na katika kuchangia maoni yake ili kufikia uamuzi wa pamoja na kwamba ataunga mkono maamuzi hayo na kuyatolea maelezo kwa wadau na washikadau wengine;

(h) kufanya maamuzi bila upendeleo na kulingana na stahili ya jambo linalofikiriwa bila kushawishiwa na mtu yeyote k.m. wakati wa kuamua mambo yanayohusu ajira, mikataba au katika kupendekeza watu watakaopewa tuzo au stahili yoyote;

(i) kuhakikisha kuwa habari zote za siri zinazohusu watu zinahifadhiwa kwa mujibu wa sheria na kwa maslahi ya umma na kutozitumia habari hizo kwa maslahi yake binafsi;

(j) kutoshiriki katika majadiliano wala katika kupiga kura katika jambo lolote ambalo anayo maslahi yake binafsi;

(k) kutoa taarifa kwenye mkutano wa Halmashauri au mkutano wa Kamati ya Halmashauri kuhusu maslahi yake binafsi katika jambo lolote linalohusu utekelezaji wa majukumu yake; na

(l) kuheshimu nafasi na hadhi ya madiwani/watumishi wenzake kwa namna itakayojenga hali ya kuheshimiana kati ya Madiwani na watumishi wa Halmashauri.

## Sifa za Tabia Binafsi

9. Kanuni Na.8 mpaka 11 zinaeleza sifa za binafsi ambazo kila Diwani atapaswa kuwa nazo ikiwa ni pamoja na:

- kuwa mwadilifu na mu-wazi wakati wote (Kanuni ya 8)
- kuzingatia kiwango cha juu kabisa cha uadilifu (Kanuni ya 9); na
- kutokuwa na uhusiano wa kimapenzi usiokubalika kati yake na madiwani wenzie au na watumishi wa Halmashauri (Kanuni ya 10)
- kutotumia vibaya dhamana na imani aliyo nayo kwa umma (Kanuni ya 11).

## Tabia ya Hadharani na Utekelezaji wa Majukumu ya Umma

10. Kanuni Na.12 mpaka 18 zinahusu maadili ambayo diwani atatakiwa kuzingatia katika utekelezaji wa majukumu yake kama mwakilishi na mtumishi wa umma. Maadili hayo ni pamoja na:

- Kuzingatia sheria, kanuni na taratibu (Kanuni ya 12).
- Kuendeleza mashauriano na kuchochea maendeleo katika ngazi za chini za Serikali za Mitaa (Kanuni ya 13).
- Kuepuka migongano ya kimaslahi (Kanuni ya 14 hadi 16).
- Kutotumia nafasi yake ya Udiwani kujinufaisha kifedha, kibiashara, au kwa namna yeyote nyingine, na kutotumia nafasi hiyo kutetea maslahi yake au ya kikundi chochote na hivyo kuathiri jukumu lake la kutoa kipaumbele katika maslahi ya umma kwa ujumla (Kanuni ya 17).
- Kutoomba na kutopokea hongo au zawadi kutoka kwa mtu anayemhudumia (Kanuni ya 18).

## Mali, Mapato na Madeni

11. Kanuni ya 19 inasisitiza kuwa diwani lazima awe na shughuli inayomwezesha kuendesha maisha yake kwa kuwa na shughuli inayompa kipato cha kutosha. Aidha, Kanuni ya 20 inamtaka diwani atangaze mali aliyo nayo yeye na mwenzie wa ndoa na watoto wao walio chini ya umri wa utu uzima, na kuhakikisha kwamba matangazo hayo yanahifadhiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri yake kwenye rejesta maalumu itakayofunguliwa kwa minajili hiyo na ambayo itakuwa wazi kukaguliwa na wananchi bila malipo. Iwapo pana mabadiliko katika hali ya mali, mapato na madeni yake, diwani atapaswa kufanya marekebisho kwenye matamko ya awali kwa kutoa matamko ya nyongeza.

## Madaraka ya Kisiasa, Uwajibikaji, Maslahi na Kinga

12. Kanuni ya 21 inamtaka Diwani:

- Asitumie nafasi na uwezo wake wa kisiasa kujipatia fedha au huduma ambazo hazikuidhinishwa na kuwekwa katika bajeti ya Halmashauri.
- Asishawishi Madiwani wengine kufikia maamuzi kuhusu masuala yanayohusu watumishi.
- Asiwabague watu kwa sababu za kisiasa, dini, jinsia, rangi au kabila.
- Asifanye shughuli yoyote ya kisiasa itakayozorotesha ufanisi au kusababisha usimamizi na utendaji mbovu.
- Kuzingatia haki na malengo yaliyowekwa na ataongozwa na ukweli wa mambo na ushauri wa kitaaluma utakaotolewa na menejimenti ya

Halmashauri na ataepuka kusukumwa na itikadi pamoja na hisia zake binafsi wakati wa kujadili na kuamua masuala yanayohusu ustawi na maendeleo ya wananchi.

13. Kanuni ya 22 hadi 24 zinazungumzia masuala yanayohusu:

- Uwajibikaji wa Diwani kwa wapiga kura na kwa wananchi kwa ujumla (Kanuni ya 22).

- Matumizi ya mali za Halmashauri zilizo chini ya dhamana ya diwani (Kanuni ya 23) – kwamba zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

- Uhuru wa kujieleza katika mikutano ya Halmashauri na Kamati zake (Kanuni ya 24) – kwamba usivunje taratibu za mjadala zilivyofafanuliwa katika Kanuni za Kudumu.

## Uhusiano Baina ya Madiwani na Watumishi wa Halmashauri

14. Vifungu 25 hadi 28 vinaelezea misingi itakayoongoza mahusiano kati ya madiwani na watumishi wa Halmashauri na kusisitiza kuwa:

- Maamuzi, maelekezo, amri na miongozo itatolewa katika **vikao** vya Halmashauri na kuelekezwa kwa Mkurugenzi kwa utekelezaji na, kwamba Diwani akiwa peke yake hatatumia nafasi yake kama mjumbe kumzuia mtumishi au wakala wa Halmashauri kutekeleza maamuzi ya Halmashauri au maamuzi ya Kamati ya Halmashauri (Kanuni ya 25).

- Madiwani na watumishi wa Halmashauri watatakiwa kujenga uhusiano mzuri utakaohakikisha ufanisi na utendaji bora katika Halmashauri, na kuepuka uhusiano wa karibu sana na watumishi wa Halmashauri unaoweza kuathiri au kudhalilisha upande wa madiwani au upande wa watumishi wa Halmashauri (Kanuni ya 26).

- Madiwani wasijihusishe na majukumu ya kitaaluma na kitaalam yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Halmashauri (Kanuni ya 27).

- Madiwani wasitoe taarifa za uongo au ushauri mbaya kwa Halmashauri ambao unaweza kuiletea Halmashauri hasara (Kanuni ya 28) na hatimaye kumfanya diwani awajibishwe kwa kulipa gharama ya hasara iliyopatikana.

## Utoaji wa Taarifa

15. Kifungu cha 29 kinamzuia Diwani kutoa taarifa za siri anazozipata kutokana na wadhifa wake ambazo hazitakiwi kutolewa kwa mujibu wa

Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 na kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa chini ya sheria hiyo.

## Uvunjaji wa Maadili na Utaratibu wa Utekelezaji wa Kanuni za Maadili

16. Kanuni ya 30 inaorodhesha makosa ya ukiukaji wa maadili. Kanuni ya 31 inahusu Kamati ya Maadili ambayo itaundwa na kila Halmashauri; na Kanuni za 32 hadi 35 zinafafanua utaratibu wa kuwasilisha malalamiko dhidi ya madiwani, kushughulikia malalamiko hayo na maamuzi yanayoweza kufanywa kutokana na malalamiko hayo.

    - Kwa mujibu wa Kanuni ya 32 mtu yeyote, awe Diwani, mtumishi wa Halmashauri, au mwananchi wa kawaida anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Katibu wa Kamati ya Maadili dhidi ya Diwani ambaye anatuhumiwa kuvunja Kanuni za Maadili ya Madiwani;
    - Baada ya kupokea malalamiko hayo Katibu wa Kamati ya Maadili atayawasilisha malalamiko hayo kwa Kamati inayoshughulikia maadili ambayo itayachambua na kuyachukulia hatua inayostahili (Kanuni ya 33 na 34);
    - Kamati ikiona kuwa tendo linalolalamikiwa linahusu uvunjaji wa sheria, basi itawasilisha shauri hilo kwa chombo kinachoshughulikia utekelezaji wa sheria husika;
    - Kwa malalamiko mengine yanayohusiana na uvunjaji wa Kanuni hizi, Kamati baada ya kujadili malalamiko yaliyoletwa itatoa mapendekezo yake kwa kikao cha Halmashauri ambacho kitatoa maamuzi yake kadiri inavyostahili (Kanuni ya 35).

17. Kanuni ya 35 inaorodhesha adhabu zinazoweza kutolewa na Halmashauri dhidi ya Diwani aliyekiuka Kanuni za Maadili. Adhabu hizo ni pamoja na:

    - Kutoa onyo rasmi;
    - Onyo la pili;
    - Kumtoza diwani;
    - Kumshtaki diwani;
    - Kumtaja diwani kwenye Taarifa ya Uwajibikaji wa Halmashauri inayopaswa kutolew katika mkutano wa mwaka wa Halmashauri.

18. Kifungu cha 36 kinatoa nafasi kwa mtu asiyeafikiana na adhabu aliyopewa kukata rufaa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya uamuzi kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

## Hitimisho

19. Kanuni za Maadili ya Madiwani zinaweka na kufafanua maadili yanayotakiwa kuzingatiwa na madiwani.  Lakini ingefaa ikumbukwe kuwa maadili ni tabia na pia ni mwenendo.  Kinachotakiwa ni kiongozi kuwa mfano wa uadilifu na uaminifu na wakati wote kuweka mbele maslahi ya umma badala ya maslahi yake binafsi.

20. Diwani akifanya kazi zake kwa uadilifu na uaminifu, na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, atajiletea heshima yeye mwenyewe na pia Halmashauri yake.

21. Maadili ya viongozi wa umma kwa nchi yoyote ni jambo muhimu linalowahusu viongozi wote bila kujali tofauti zao za kiitikadi.  Vyama vya siasa vinaweza kutofautiana kisiasa, kiitikadi na hata kimtazamo na hivyo kuwa na sera tofauti, lakini machoni mwa wananchi kinachotazamiwa ni uadilifu wa viongozi bora na ubora wa huduma zinazotolewa na viongozi wao.

22. Madiwani wanatakiwa kutoa mfano bora wa uadilifu ikiwa ni pamoja na kutojihusisha kabisa na rushwa.  Kwa kufanya hivyo wanaweza kusimamia maadili kwa wale walio chini yao.